

Namna ya swala ya mtume (s.a.w). na Namna ya kutawadha

Abdul Aziz bin Abdullah bin Baaz

Kitabu hii kinalezea sifa ya swala ya mtume (s.a.w). na jinsi ya kutawadha, kitabu hiki nizawadi kwa waislam wote wanaotaka kumuiga mtume (s.a.w) katika swala na udhu.

<https://islamhouse.com/2783774>

-
- Ndugu Yangu Kwa Mfano Wa Siku Hii Ya Qiyama Fanya Mema
 - Utangulizi:
 - Ndugu Yangu

- Kwa Mfano Wa Siku Hii Ya Qiyama Fanya Mema
 - Siku Ya Kutolewa Roho
 - Siki Ya Kuingizwa Kaburini
 - Siku Ya Kufufuliwa

Ndugu Yangu Kwa Mfano Wa Siku Hii Ya Qiyama Fanya Mema

Utangulizi:

Hakika sifa zote njema ni za Mwnyezi Mungu ambae tuna muhimidi, tunamuomba msaada na msamaha na tunajikinga kwake kutohana na shari za nafsi zetu na matendo yetu mabaya, mwnye kuongozwa na Mwenyezi

Mungu hakuna wa kumpoteza na mwenye kupotezwa na Mwenyezi Mungu hakuna wa kumuongoa, na ninashahidilia kuwa hakuna Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika. Na ninashahidilia kuwa Muhammad (s.a.w) ni mja wake na Mtume wake.

Ndugu Yangu

Kwa Mfano Wa Siku Hii Ya Qiyama Fanya Mema

Amesemaa Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika kwa Mola wako Mlezi ndio marejeo}. (Al-Alaq: 8).

Katika kitabu cha Mwenyezi Mungu kuna aya inayopasua maini na nyoyo za waja wa Mwenyezi Mungu wakweli zinainyenyeka aya hiyo, muumini wa kweli mwenye itikadi sahihi na yakini anapoizingatia aya hiyo moyo wake unatekwa na akili itashughulishwa na aya hiyo, **na aya hiyo itakuwa ndiyo hima yake:** Hakika ni aya ya kukhofisha na ni ukulele wa kutahadharisha, inakhofisha siku ambayo siyo kama masiku mengine na inazungumzia tukio la kufufuliwa watu wote.

Ni aya ambayo kwa sababu yake Mwenyezi Mungu alituma Mitume na akateremsha Vitabu na ndani ya siku hiyo watu watatengana, kundi moja

litaingia Peponi na kundi jingine
litaingia Motoni, **aya hiyo ni kauli ya**
Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na
iogopeni Siku ambayo mtarudishwa
kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila
nafsi italipwa ilicho chuma. Nao
hawatadhulumiwa}. (**Al-Baqra: 281**).

Hakika ni siku ambayo kila nafsi
itarejea kwa Mola na Muumba wake!
Hikika ni siku ambayo nafsi
zitahesabiwa na kila nafsi itahesabiwa
kulingana na matendo yake, **amesema**
Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Basi
anaye tenda chembe ya wema,
atauona!* Na anaye tenda chembe ya
uovu atauona!}. (**Al-Zilzaal 7-8**).

Ndugu yangu: Hakika siku hiyo ni siku ya Qiyama, siku ambayo Mitume watafazaika na maneno yao siku hiyo yatakuwa (**Allahuma sallim sallim**), mawalii watatetemeka siku hiyo kwa khofu na uwoga ni siku ya shida na tabu, siri zitafichuliwa siku hiyo na vitabu vya matendo vitagawiwa na viumbwe watakuwa ktika fitna siku hiyo, amesema **Mwenyezi Mungu Mtukufu**: {Siku hiyo mtahudhurishwa-haitafichika siri yoyote yenu}. (**Al-Haaqah: 18**).

Ni siku ambayo watasimamishwa mashahidi, kuna nyuso siku hiyo zitakuwa nyeusi na nyingingine zitakuwa nyeupe, amesema **Mwenyezi Mungu Mtukufu**: {Siku ambayo kila

nafsi itakuja jitetea, na kila nafsi
italipwa sawa sawa na a'mali ilizo
zifanya, nao hawatadhulumiwa}. (Al-
Nahli: 111).

Ni siku ambayo mtoto atamkimbia
baba yake na atamkana mama yake na
ndugu yake na mkewe na mwanae,
amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:
{Kila mtu mionganini mwao siku hiyo
atakuwa na lake la kumtosha}. (Abasa:
37).

Ni siku ya malipo na ni siku ya majuto,
ni siku ya kubadilisha na ni siku ya
mkutano, ni siku inayosogea na ni siku
ya marejeo, ni siku ya hukumu na ni
siku ya kupimwa matendo, ni siku ya
kukata tamaa na ni siku ngum, ni siku

ya kushuhudiwa na ni siku ya upambanuzi, ni siku ya kukimbiana na ni siku ambayo haina shaka ndani yake, ni siku isiyozuulika kwa Mwenyezi Mungu na hakuna nafsi itakayo zungumza isipokua kwa idhini yake Mwenyezi Mungu, sauti zitakuwa kimya kwa Mwenyezi Mungu hautosikika isipokuwa mnong'ono, kila mmoja siku hiyo atatarajia amani ya nafsi yake wala hatomjali aliye pembezoni mwake, **atakua akisema:** Nafsi yangu! Nafsi yangu!.

Ndugu yangu uko wapi wewe na siku hii? Ziko wapi kumbukumbu zako kutokana na hali ya siku hiyo? Iko wapi hima yako kutokana na mfazaiko wa siku hiyo na vitisho vyake!?.

Kutoka kwa Abuu Huraira (رضي الله عنه).a) alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Watu watatokwa na jasho siku ya Qiyama mpaka jasho zao zitafika ardhini kiasi cha dhira sabini, na jasho litawameza mpaka kufikia katika masikio yao). Ameipokea hadithi hii Imamu Bukhar.

Amesema Ibrahim Al-Tamimy: [Vitu viwili vilinikatia ladha ya dunia: Kukumbuka Umauti na kukumbuka kusimamishwa mbele ya Mwenyezi Mungu].

Anasema Mshairi:

Ipigie mfano nafsi yako ikighafilika na umauti,

Itakavyokuwa siku ya Qiyama wakati
mbingu inaondoka

Na wakati juu litakapo kunjwa kunjwa
na likasogezwa

Karibu na vichwa vya wanadamu.

Na pindi nyota zitakapo dondoka na
zikazunguka badala

Ya kuwaka. Na bahari zitakapo ripuka
kutokana na khofu

Utaziona kama moto mkubwa
unavyowaka.

Na kumbuka milima itakapong'oka
ikatoka sehemu yake,

Utaiona kama mawingu
yanavyotembea.

Na pindi vitakapo gawiwa vitabu vya matendo,

Siri zote za wanadamu zitafichuka.

Na kumbuka mwanadamu Moto wa Jahannam utakapo washwa

Basi utakuwa ukiunguruma kwa ajili watu wenyewe madhambi.

Ndugu yangu: Kila kitu kina uhakika wake, na uhakika wa imani yako kwa siku hii ni kuibeba hima yako ndani ya moyo wako kutokana na siku hiyo na mawazo yako yaifanyie kazi siku hiyo, na uikumbuke mara kwa mara kwasababu ni siku ngum na kwa makafiri siyo nyepesi, amepata hasara mwenye kubeba dhulma siku hiyo na

mwenye kughafilika na siku hiyo amepata hasara, **amesema Mwenyezi Mungu Mtukfu:** {**(Aambiwe)**: Kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya; basi leo tumekuondolea pazia lako, na kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.}. **(Qaaf: 22).**

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukfu: {Basi nyinyi abuduni mpendacho badala yake Yeye. **Sema:** Hakika walio khasirika ni wale walio jikhasiri nafsi zao na ahali zao Siku ya Kiyama. Tambueni kuwa hiyo ndiyo khasara iliyo dhaahiri}. **(Al-Zumar: 15).**

Anasema Mshairi:

Ewe kijana mwenye kumuasi Mola wa A'rshi hivi unajua malipo ya mwenye maasi? Bisi ni Moto wa Jahannam wenyе muungurumo na hasira siku atakapochukuliwa mwenye maasi na kutupwa ndani yake.

Ikiwa unaweza kuvumilia moto basi muasi Mwenyezi Mungu, na la sivyo usimuasi Mwenyezi Mungu, na yale uliyoyachuma katika maasi ilazimishe nafsi yako kuyaacha.

Siku Ya Kutolewa Roho

Ndugu yangu: Qiyama cha mtu kinasimama kwa kufa kwake, wakati huo ndio itaonekana nafasi yake na mafikio yake yatabainika, siku ya kufa kwake siri inafichuka na kubainika

namna alivyo na matendo yake
yanabainika hali yake, sifa yake na
malipo yake yana nasibiana na
matendo aliyoafanya katika uhai
wake.

Wakati wa kutokwa roho: Ni wakati wa kuachana unaoshuhudiwa, ni wakati mwanadam anajionea ulimwengu wa ghaibu, basi anashuhudia na kuona Malaika wakimjia vile walivyo kutokana na matendo aliyonayo, na katika hadithi amesema Mtume (s.a.w):
(Anapokaribia kufa muumini wanamjia Malaika wa rehma na Hariri nyeupe kisha wanasema kuiambia roho toka ukiwa umeridhia na umeridhiwa uende katika raha na manukato na

Mola wako hajakukasirikia, baisi ile inatoka ikiwa na harufu nzuri ya miski wanapeana Malaika baadhi yao kwa wengine mpaka wanaifikisha katika mlango wa mbingu kisha Malaika wanasesma uzuri ulioje wa harufu hii mliyokuja nayo kutoka ardhibjini! Kisha wanaiweka katika roho za waumini, basi hao waumini wanamfurahia kuliko anavyomfurahia mmoja wenu mgeni anapo mtembelea, kisha wanamuuliza Fulani kafanya nini? na Fulani kafanya nini? Wengine watasema muacheni hakika alikuwa katika matatizo ya dunia, atakaposema kuwajibu atasema je! Hakuja huku? Watajibu aliyelekwa katika mafikio yake ya Motoni. Na hakika makafiri wanapofikiwa na umauti wanajiwa na

Malaika wa adhabu na kitambaa chepesi kisha wanasema kuiambia roho: toka haliyakuwa umechikia na umechukiwa uende kataka adhabu ya Menyezi Mungu, itatoka ikiwa na harufu mbaya kama ya mzoga, wataipeleka mpaka katika mlango wa ardhini watasema ubaya ulioje wa harufu hii? Kisha waiweke katika roho za makafiri).

Ndugu yangu: Mtu mwenye akili anazingatia mwisho wake na anaufanyia maandalizi mazuri, basi itakase nafsi yako kwa kufanya twaa, na itie manukato roho yako kwa kumridhisha Mola wako na kutekeleza amri zake na kujiepusha na makatazo yake, na kufanya haraka katika

kutenda mambo ya kheri ikiwa inatarajia kuokoka siku itakapotolewa na kunyanyuliwa daraja wakati wa kufariki, hakika ya roho hazipati manukato isipokuwa kwa amali njema ambazo ndani yake ni kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kujiepusha na ushirikina, **anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** {Hakika shirki ni dhulma kubwa}. (Luqman: 13).

Matendo mazuri pia yanakusanya tabia nzuri na ibada zilizo sahihi ambazo zinafanywa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, **mfano wa roho kama hizi Mwenyezi Mungu amezizungumzia katika Qur'an kwa kusema:** {Wale ambao Malaika huwafisha katika hali njema, **wanawaambia:** Amani iwe juu

yenu! Ingieni Peponi kwa sababu ya
yale mliyo kuwa mkiyatenda}. (Al-
Nnahli: 32).

Roho kama hizi ndiyo
zitakazopokelewa na walinzi wa Pepo
na huku wakisema: {Na walio mcha
Mola wao Mlezi wataongozwa
kuendea Peponi kwa makundi, mpaka
watakapo fikilia, nayo milango yake
imekwisha funguliwa. **Walinzi wake**
watawaambia: Salaam Alaikum,
Amani iwe juu yenu! Mmet'ahirika.
Basi ingieni humu mkae milele}. (Al-
Zzumar: 73).

Ndugu yangu: Katika kutokwa na roho
ukweli wa matendo huwa unadhihirika
na kubainika udhalili wa dunia, kwani

hakuna kinachodhihiri kwa anayekufa chenye kumfaa isipokuwa isipokuwa matendo yake, na kwa kufa kwake ndiyo mwisho wa matendo yake, na kutokana na matendo atakayokufa nayo ndiyo atakayofufuliwa kwayo, kama ilivyokuja katika hadithi ya Mtume (s.a.w): (**Mwenye kufa katika jambo, atafufuliwa katika jambo hilohilo**). Ameipokea Haakim.

Ikiwa ni hivo ndugu yangu, wakati roho yako inatoka inaonyesha hali yako itakavyokuwa kaburini, siku ya kufufuliwa na siku ya kuhesabiwa, **mtu mmoja aliambiwa wakati anakata roho:** sema laa ilaha ila Llah! Akasema: sitonufaika na kauli hiyo, na mimi hakuna dhambi ambayo sijaifanya,

kisha akakata roho na hakuweza
kuitamka.

Na mtu mwingine aliambiwa: sema laa
ilaha ila Llah! Akasema: haitanisaidia,
sijawahi kuswali hata swala moja,
kisha akakata roho na hakuweza
kuitamka.

Na mtu mwingine aliambiwa: sema laa
ilaha ila Llah! Akasema kila
ninapotaka kutamka ulimi wangu
unagoma kutamka.

Basi watu hao walizama katika maasi
wakaitelekeza shahada na wakawa na
mwisho mmbaya, tunamuomba
Mwenyezi Mungu atupe salama.

Anasema Mshairi:

Utaacha ibada kwa ajili ya
kujishughulisha na dunia mpaka lini!

Utakuwa mvivu wa kuacha
ibada mpaka lini!

Kila siku maovu yako
yanaandikwa wewe huchoki?

Ewe mwenye kuiadhibu nafsi
yako,

Na unachelewa kuwa mtu
mwema.

Basi juu kuwa kifo kinakujia
haraka

Na kaburi ndio sanduku la
matendo.

Ndugu yangu fahamu ya kwamba
hakika mwanadamu madamu
anamatumaini ya maisha basi hawezi
kuyakata matumaini yake ya kidunia,
na huenda nafsi yake isimkubalie
kuacha ladha za dunia na matamanio
yake sawa ni ya halali au ya haramu na
shetani anaipa matarajio ya kutubia
mwisho wa umri wake, kifo kinapofika
na akakata tamaa ya maisha ndipo
anapozinduka na kujua kwamba
alikuwa katika dimbwi la matamanio
ya dunia, na wakati huo ndipo
anapojuta majuto makubwa
yanayokaribia kuiangamiza nafsi yake,
na ndipo anapoomba kurejea duniani
ili atubie na kufanya matendo mema,
wakati huo ombi lake halitojibiwa, basi
yatajikusanya kwake mambo mawili,

uchungu wa kutokwa na roho na
majuto ya kutokufanya mema.

Mwenyezi Mungu Mtukufu
amewatahadharisha waja wake
kutokana na hali hiyo ili wajiandae na
umauti kabla haujawafikia kwa
kufanya toba na matendo mema,
amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:
{ Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na
silimuni kwake, kabla ya kukujieni
adhabu. Kisha hapo
hamtanusuriwa*Na fuateni yaliyo bora
kabisa katika yale yaliyo teremshwa
kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi,
kabla haijakujieni adhabu kwa ghafla,
na hali hamtambui*Isije ikasema nafsi:
Ee! majuto yangu kwa yale niliyo
poteza upande wa Mwenyezi Mungu,

na hakika nilikuwa miongoni mwa wanao fanya maskhara!}. (Al-Zzumar: 54-56).

Alisikika mmoja katika watu waliokuwa wakitokwa na roho akijipiga usoni mwake huku akisema:
Ee majuto yangu kwa yale niliyo poteza upande wa Mwenyezi Mungu,
na hakika nilikuwa miongoni mwa wanao fanya maskhara.

Na akasema mwingine wakati wa kufa kwake: dunia imenishughulisha mpaka umri wangu umeondoka.

Na akasema mwingine wakati wa kufa kwake: yasikudanganyeni maisha ya dunia kama yalivyo nidanganya mimi,
amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{ Mpaka yanapo mfikia mmoja wao mauti, **husema:** Mola wangu Mlezi! Nirudishe* Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyo yaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku watapo fufuliwa}. (**Al-Muuminun:** 99-100).

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: { Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, **tena hapo akasema:** Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?* Wala Mwenyezi Mungu hataiakhirisha nafsi yoyote inapo fika ajali yake; na Mwenyezi

Mungu anazo khabari za mnayo
yatenda}. (Al-Munafiquun: 10-11).

Na amesema Mwenyezi Mungu
Mtukufu: {Na watatiliwa kizuizi baina
yao na hayo wanayo yatamani, kama
walivyo fanyiwa wenzao zamani.
Hakika hao walikuwa na shaka ya
kutia wasiwasi}. (Sabaa: 54).

Jopo la wanachuoni wema
waliotangulia akiwemo Omar bin
Abdul-Aziz wameifasiri aya hii
kwamba, hao watu waovu waliotajwa
katika aya waliomba toba wakati
milango ya toba imeshafungwa.

Amesema Al-**Hasan**: Muogope
Mwenyezi Mungu ewe mwanadamu,
yasikupate wewe mambo mawili,

uchungu wa mauti na majuto ya kutokufanya mema.

Amesema Ibn Samak: Tahadhari na uchungu wa mauti na mshangao, kwa kifo kukujia ghafla hali ya kuwa upo katika upotofu, utakayoyapata na utakayoyaona miongoni mwa adhabu hayana mfano wake. (**Latwaaif Al-maarif, cha Ibn Rajab, ukurasa wa 575**).

Siki Ya Kuingizwa Kaburini

Siku hiyo ndugu yangu kuonekana kwa mtu duniani kutaisha, ndugu zake watambeba wakiwa wanalia, watamuweka kaburini na kumfukia na mchanga, na watacaa siku chache wakihuzunika na kisha watamsahau.

Ama aliyezikwa, kwa hakika ameingia katika ulimwengu wa barzakh, na amekalishwa tangu kuingia kwake kaburini kwa ajili ya kuulizwa,
amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:
{Basi anaye tenda chembe ya wema,
atauona*Na anaye tenda chembe ya
uovu atauona!}. (**Al-Zzilzaal: 7-8**).

Sogea karibu ndugu yangu tuishi na mawaidha ya Mtume (**s.a.w**) yanayobainisha mafikio ya mwanadamu katika kaburi lake, na yanatupa habari juu ya yale yanayojiri katika kaburi kutokana na mambo tusiyoyajua, anasema Mtume (**s.a.w**): (**Hakika maiti anapolazwa kaburini, anasikia nyayo za waliomsindikiza pindi wanaporudi, akiwa ni muumini**

swala yake inakuwa katika kichwa chake, na swaumu inakuwa upande wake wa kulia, na zaka inakuwa upande wake wa kushoto, na matendo yake ya kheri miongoni mwa sadaka, swala, wema na kuwafanyia watu mambo mazuri, yanakuwa miguuni mwake, **swala itasema:** upande wangu hakuna nafasi ya kuingia, **na swaumu itasema:** upande wangu hakuna nafasi ya kuingia, **kisha zaka itasema:** upande wangu hakuna nafasi ya kuingia, **na matendo yake mema yaliyo upande wa miguuni yatasema:** upande wangu hakuna nafasi ya kuingia, **kisha antambiwa akae!** Naye atakaa, **utaletwa mfano wa jua na atatoa idhini lizame,** **kisha ataulizwa:** unaonaje kuhusu huyo aliyekuwa kabla yenu

unaselaje kuhusu yeye na unamshahidilia nini? Atasema: niacheni mpaka niswali. **Kisha watamwambia:** hakika utaswali tujibu tunayokuuliza. Unaonaje kuhusu huyo aliye kuwa kabla yenu unaselaje kuhusu yeye na unamshahidilia nini? **Mtume (s.a.w)** akasema: yule mtu atasema: Muhammad! Ninashahidilia kuwa ni Mtume wa Mungu, na hakika alikuja na haki kutoka kwa Mola wake, **kisha ataambiwa:** wewe uliishi katika imani hiyo, na ulikufa na imani hiyo, na utafufuliwa na imani hiyo Mwenyezi Mungu akipenda, kisha atafunguliwa mlango miongoni mwa milango ya Pepo, **na kisha ataambiwa:** haya ndiyo makazi yako na ndiyo aliyokuandalia Mwenyezi Mungu.

Basi atazidi kuwa na tamaa na furaha,
kisha litapanuliwa kaburi lake dhira
sabini na litatiwa nuru ndani yake na
kiwiliwili kitarejeshwa kama
kilivyokuwa mwanzo, na inawekwa
roho yake katika roho za watu wema
mfano wake, zinakuwa kama ndege
waliowekwa katika miti ya Peponi, **na**
hiyo ndio maana ya kauli ya Mwenyezi
Mungu Mtukufu: {Mwenyezi Mungu
huwatia imara wenye kuamini kwa
kauli ya imara katika maisha ya dunia
na katika Akhera}.(Ibrahim: 27).

Na hakika kafiri atakapojiwa na
Malaika katika kaburi lake upande
wake wa kichwani, kuliani mwake,
kushotonii mwake na miguuni mwake
hawatakuta kitu chochote katika

matendo mema, **kisha ataambiwa akae!**
Naye atakaa akiwa mwoga na huku
akitetemeka kisha ataulizwa: Unaonaje
kuhusu huyo aliyekuwa kabla yenu
unasemaje kuhusu yeye na
unamshahidilia nini? Atajibu: Mtu
gani? Na wala hatajua jina lake,
ataambiwa Muhammad! Atajibu: sijui!
Nilikuwa nikisikia watu wakisema
nami nikasema kama wanavyosema,
kisha ataambiwa: wewe uliishi katika
imani hiyo, na ulikufa na imani hiyo,
na utafufuliwa na imani hiyo
Mwenyezi Mungu akipenda, kisha
atafunguliwa mlango mionganini mwa
milango ya Moto, **na kisha ataambiwa:**
haya ndiyo makazi yako ya Motoni na
ndiyo aliyokuandalia Mwenyezi
Mungu, basi atazidi kuwa na majuto na

maangamio, kisha atafunguliwa mlango miongoni mwa milango ya Pepo na ataambiwa haya ndiyo makazi yako aliyokuandalia Mwenyezi Mungu laiti kama ungemtii, basi atazidi kuwa na majuto na maangamio, kisha atabanwa katika kaburi lake mpaka mbavu zake zitofautiane, **hayo ndiyo maisha ya dhiki aliyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenyeye dhiki}. (Twaha: 124).

Ndugu yangu: Jiandae kwa ajili ya kuulizwa na kukutana na vitisho hivyo, hakika kaburi ni nyumba ya kwanza ya akhera, na ndani yake utadhihiri ukweli wa matendo.

Othman bin Affaan (رضي الله عنه) alikua akisimama katika makaburi analia mpaka ndevu zake zinalowa,
akaulizwa: Mbona unapokumbuka Pepo na Moto hulii lakini unaposimama makaburini unalia?
Akasema: Nilimsikia Mtume (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ)
akisema: (*Hakika kaburi ni nyumba ya kwanza ya akhera, atakapookoka mtu kaburini basi yatakayokuja baada yake ni mepesi, na ikiwa hakuokoka kaburini basi yatakayokuja baada yake ni mazito.*)

Basi anajiandaa na ibada kutokana na siku kama hii mtu mwenye akili, ndani ya kaburi mwenye matendo mema atapata mafanikio na matendo maovu atapata hasara.

Siku Ya Kufufuliwa

Ndugu yangu fanya ibada kwa ajili ya siku hii ya kufufuliwa kwasababu ukombozi wa nafsi yako siku hiyo ni matendo yako mema, **amesema**

Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Wala hapana yeote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia. Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe* Kisha tutawaokoa wale walio mchamngu; na tutawaacha madhaalimu humo wamepiga magoti}. (Mariyam: 71-72).

Mali zako siku hiyo hazita kufaa na dini yako hautoinunua kwa mali zako siku hiyo, na cheo chako siku hiyo hakitakunyanyua, **amesema Mwenyezi**

Mungu Mtukufu: {Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana* Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi}. (Al-Sshuaraa: 88-89).

Na amesema Mtume (s.a.w): (Siku ya Qiyama ataambiwa mtu wa Motoni: Unaonaje laiti ungekuwa unamiliki vilivyoko ardhini ungevitoa fidia ili uokolewe na huu Moto? Atajibu: Ndiyo! Mwenyezi Mungu atamwambia: Umesema uongo! Nilitaka kwako wewe jepesi kuliko hilo, nilikukataza toka ukiwa katika mgongo wa Adam ya kwamba usinishirikishe na chochote, ukakataa na ukashirikisha). (Swahihul-Jaamia: 8123).

Ndugu yangu kumbuka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kaamili Siku ya Kiyama. Na atakaye epushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu}. (Al-Imran: 185).

Na kumbuka kuwa utarejea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, **kama anavyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu:** {Hakika kwa Mola wako Mlezi ndio marejeo}. (Al-a'laq: 8).

Na utaulizwa kama anavyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na

wasimamisheni. Hakika hao
watasailiwa}. (Al-Swafaat: 24).

Basi kurejea kwako kufanyie hesabu,
na maswali yako yaandalie majibu, na
tahadhari usije ukafa katika hali ya
kughafilika ukatamani wakati huo laiti
ungezidishiwa umri kwa kusema:
{ Mpaka yanapo mfikia mmoja wao
mauti, husema: Mola wangu Mlezi!
Nirudishe* Ili nitende mema sasa
badala ya yale niliyo yaacha. Wapi!
Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na
nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku
watapo fufuliwa}. (Al-Muuminuun:
99-100).

Na rehma na amani ziwe juu ya
Mtume wetu Muhammad (**s.a.w**) na
watu wake, na Maswahaba wake wote.